BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com


# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO, MAONI NA USHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA OFISI YA RAIS IKULU

---

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuweza kusimama mbele ya Baraza hili Tukufu kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi juu ya Mapendekezo, Maoni na Ushauri uliotolewa katika ripoti ya mwaka uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi kwa uadilifu, hali inayopelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu. Kamati inaridhishwa sana na juhudi za Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake kwa kusimamia changamoto mbalimbali katika nchi yetu na kuzipatia utatuzi wake.

tunamuomba Mwenyezi Mungu kumzidishia afya njema, hekma na busara katika kuitumikia nchi yetu na kupeleka mbele gurudumu la maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Mhe. Jamal Kaasim Ali pamoja na uongozi mzima wa Ofisi hii kwa ushirikiano wao mkubwa wanaotuonesha katika kufanikisha jukumu zito la utekelezaji wa mipango ya Serikali kwa ujumla la kuwapatia huduma bora na salama wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati yetu ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna wanavyonipatia mashirikiano makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | M/Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Mussa | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *7.* | Nd. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *8.* | Nd. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Nd. Shawana Mohammed Haji | Katibu |
| *10.* | Nd. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, kwa kutumia Kanuni ya 107(3) imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia; ambapo kazi hiyo ilifanywa vyema katika kipindi kilichopita na bado Kamati itazidi kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo hayo katika kazi zake za kila siku. Ripoti hiyo hujumuisha ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Wizara na Taasisi zake ambazo ilizifanyia kazi kwa

mwaka wa fedha uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa kanuni ya *109(15)* ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la mwaka 2020 imetoa fursa ya lazima kwa kila Kamati kutayarisha ripoti ya mwaka itakayowasilishwa katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kila mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kanuni ya *109(17)* ya Kanuni hizo za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa mapendekezo hayo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara/taasisi husika kujadili utekelezaji wa ripoti iliyowasilishwa Barazani katika mkutano husika.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaelezea muhtasari wa utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati kwa Ofisi ya Rais Ikulu kutipitia ripoti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

## UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA MAONI/USHAURI WA KAMATI:

**Mheshimiwa Spika**, katika Ripoti ya Kamati kwa mwaka 2022/2023 jumla ya mapendekezo *07* yalishauriwa katika Ofisi ya Rais Ikulu. Aidha, Kamati imeridhia na inatoa shukurani zake za dhati kwa Ofisi hii kwa jinsi walivyoweza kutekeleza vyema maoni na ushauri wa Kamati, hali inayoonesha ukomavu mkubwa katika utekelezaji wake pamoja na jitihada njema za kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Ofisi kutekeleza vyema maoni na ushauri uliotolewa na Kamati, kuna baadhi ya mapendekezo Kamati imeona ni vyema kufanyiwa marekebisho ili kwenda sambamba na uhalisia wake.
Miongoni mwa mapendekezo hayo ni haya yafuatayo:

### Hoja Namba 4

"Kamati imeshauri kuwekwa mazingira mazuri ya kuimarisha hali ya ulinzi na

usalama kwa kujenga uzio wa ukuta na kuweka kamera maalumu za usalama katika makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar yaliyopo Dodoma".

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia majibu ya hoja hii Kamati imeipongeza kwa dhati Afisi ya Rais Ikulu kwa kuweza kutekeleza ushauri wa ufungaji wa Kamera maalumu za usalama. Hata hivyo, Kamati imeitaka Ofisi ifuatilie utekelezaji wa ujenzi wa uzio katika makaazi hayo kwa haraka zaidi pamoja  na kuandika upya majibu yake kama ilivyoelekezwa.

**Hoja Namba 5**

"Kamati imeshauri kufikiriwa kwa karibu na kuwekwa mipango ya kufanya ukarabati mkubwa au kujenga upya Ikulu ndogo iliyopo Bwefum ili isipoteze haiba yake".

**Mheshimiwa Spika,** kupitia hoja hii Kamati ilielekeza kutolewa ufafanuzi zaidi na kuonesha wazi hatua inayoendelea juu ya upembuzi yakinifu wa kuliendeleza eneo hili au kutafuta eneo jengine kwa ajli ya ujenzi.

**Hoja Namba 7**

"Kamati iliagiza kufanyiwa udhibiti wa mmong'onyoko wa ardhi unaoendelea kufanyika jirani na nyumba ya Mheshimiwa Rais Mstaafu wa awamu ya tano (5) Dkt. Salmini Amour Juma."

**Mheshimiwa Spika,** suala la kuwaenzi viongozi wetu wa kitaifa kwa kuwawekea mazingira bora ya makaazi yao ni suala lisiloepukika na ambalo halihitaji mjadala mkubwa kutokana na juhudi zao walizozichukua katika kulipambania Taifa. Hivyo basi, Kamati ilitoa ushauri huu baada ya kuona mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri mazingira hayo na tunaendelea kushauri Serikali kuharakisha kuchukua hatua za kudhibiti athari hizo kabla ya tatizo kuwa kubwa zaidi. Aidha, Kamati inaitaka Ofisi ya Rais Ikulu kwa kufuatilia maombi waliyotoa kwa Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) na kupata taarifa ya kitaalamu kuhusiana ufahamu wa eneo hili na namna walivyojipanga katika kuliendeleza na kunusuru zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeridhika na utekelezaji wa mapendekezo, maoni na ushauri ulioyatoa katika Ripoti iliyopita lakini jitihada zaidi zinahitajika hasa za kuwapatia maslahi bora watendaji wetu ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao. Sambamba na hayo, Kamati inashauri Ofisi hii kumaliza changamoto ya maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Rais Ikulu na Baraza la Mapinduzi ili kuleta ufanisi wa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, ni imani ya Kamati yetu kuwa kupitia utekelezaji wa Ofisi hii ni wazi kwamba umeenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mipango mbali mbali ya kimaendeleo ambapo changamoto ndogo ndogo zilizojitokeza zimepatiwa ufumbuzi kwa muda mfupi kutokana na ukomavu na ubunifu wa watendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ahsante,

................................

(**Mhe. Machano Othman Said**)
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR**